TANGAZO LA MADA YA KAMPENI YA SIKU 16 ZA UANAHARAKATI DHIDI YA DHULUMA ZA KIJINSIA

Novemba 25 - Desemba 10, 2010

MWAKANI 2010

Mwaka huu tunapoadhimisha miaka ishirini tangia kuanzishwa Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati dhidi ya Dhuluma za Kijinsia, Kituo cha Uongozi wa Wanawake Duniani (CWGL) kinatia kumbukumbu umuhimu wa juhudi hiyo kwa kutafakari nyenzo mpya za kufanikisha lengo la kampeni hii kuafikia mageuzi yenye mabadiliko ya kudumu. Kila mwaka, washiriki wapya hujiunga na kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati kuangazia dhuluma aina mbalimbali zinazowakumba wanawake katika jamii, mashinani, katika ngazi za kitaifa na ki-mataifa ulimwenguni kote. Umuhimu unaoendelea kupewa swala la dhuluma za kijinsia katika majukwaa ya kitaifa ni ishara ya juhudi dhabiti zinazotekelezwa na wanaharakati ulimwenguni kote. Licha ya hamasisho, wanawake wangali wanadhulumiwa kwa idadi kubwa huku aina za dhuluma mamboleo zikijitokeza. Kwa hivyo, sote walinda-haki za wanawake tunawajibika kuangazia kwa makini miundo inayoruhusu dhuluma za kijinsia kuwepo na kuendelezwa. Basi, baada ya kushauriana na wanaharakati, mashirika na wataalamu kote ulimwenguni, Itikadi-Jeshi imetambuliwa kuwa mojawapo ya miundo dhalimu katika kuendeleza dhuluma dhidi ya wanawake.

Ingawa kunazo tafsiri na mawazo mbalimbali kueleza Itikadi-Jeshi, katika kampeni hii tunachukulia muundo huu kumaanisha "falsafa inayobuni tamaduni za uoga kwa waadhiriwa, na hutegemea utumizi wa mabavu, vita au mbinu za kijeshi kusuluhisha mizozo na kutekeleza malengo ya kibinafsi ya ki-uchumi na ya ki-siasa". Ni itikadi inayoadhiri usalama na ulinzi kamili na wa kudumu kwa wanawake na jamii kwa jumla. Itikadi-Jeshi ni falsafa nyeti inayoshawishi mtazamo na jinsi tunavyouhisi ulimwengu; inashawishi jinsi tunavyowaona majirani zetu, jamii zetu, maisha ya umma; na jinsi tunavyowahisi binadamu wenzetu duniani. Kuikumbatia Itikadi-Jeshi huelekeza uwepo wa watesi-maadui kote kote, na zaidi kukubali kuwa utumizi wa nguvu ni mbinu halisi kushurutisha na kusuluhisha maswala tata, na kutatua shida ulimwenguni. Tukiipa kisogo itikadi hii, tusipoipinga itikadi hii, basi itakuwa tunapalilia ubabe, mifumo duni ya ki-mamlaka, na kuwapa nafasi wanaodhulumu wanawake katika hali ya kivita kutochukuliwa hatua za kisheria. Bali, kuukomesha muundo huu kutawatia motisha na fursa ya kubuni mawazo mwafaka ya ki-usalama kuwajumuisha wanawake katika utumishi wa umma; kutatuwezesha kuutengeza ulimwengu usiotegemea ubora wa majeshi na uuzaji wa zana za kivita, ila ulimwengu wenye msingi wa mahusiano ya uaminifu na ushirikiano.

Ni muhimu kuangazia Itikadi-Jeshi katika jamii zote ulimwenguni. Madhara yanayotokana na Itikadi-Jeshi ya ki-mali, ki-vyuo, ki-tamaduni, ki-saikologia ni mengi na wala hayakadiriki kwa urahisi. Vita, migororo na mizozo ya ki-ndani (nchini), ukomeshaji kimabavu makundi ya upinzani ya kisiasa na vyama vya kutetea haki za kijamii – utumizi wa nguvu ni baadhi ya matokeo ya Itikadi-Jeshi - huwa zinawalenga wanawake mara nyingi na huwaadhiri wanawake pakubwa. Ubakaji hutumiwa kama mbinu ya ki-vita kuwaogofya na kuwashusha hadhi wanawake na wamiliki wao. Hata hivyo, ubakaji ni moja tu kati ya dhuluma inayowakumba wanawake na wasichana katika hatua na viwango mbalimbali punde mizozo inapoanza, huku mizozo inapoendelea na hatimaye mizozo inapositishwa. Itikadi-Jeshi haianzii wala kuishia katika maeneo ya ki-vita; wala haiadhiri tu maisha ya umma.

Jamii za waume na pia wake wenye mawazo ya itikadi za kijeshi huenda wakajipata katika hali ya wa vita na utumizi wa silaha wanapodhulumiwa kijinsia manyumbani mwao ambako hamna kumulikwa na jicho la umma. Vile vile wanawake wanaohudumu katika jeshi hupata kuvamia kingono na wanajeshi wenzao wa kiume. Hata katika maeneo kusiko na vita moja kwa moja, huwa hayaepuki adhari za itikadi –kijeshi: hutuma wanajeshi kutengeneza au kusafirisha silaha, pia huchangia majeshi ya serikali za kigeni badala ya kuchangia juhudi za maendeleo. Serikali kama hizi huyapa majukumu duni kipa-umbele na hutumia asilimia kubwa ya raslimali katika makadirio ya fedha ya serikali kuwekeza majeshi na ununuzi wa silaha kuliko huduma za kijamii kama vile elimu, afya, usalama na uhakika wa ujira na maswala ya maendeleo ambayo yangeleta manufaa chungu nzima kwa wanawake. Kutokana na sababu hizi, mada ya kimataifa ya mwaka huu wa elfu mbili na kumi katika kampeni ya siku kumi na sita itakuwa:

MIUNDO YA DHULUMA: UCHAMBUZI WA MIINGILIANO KATI YA UJESHIJESHI NA DHULUMA DHIDI YA WANAWAKE

CWGL inaruwaza kuwa mada hii kuhusu miingiliano baina ya Ujeshijeshi na Dhuluma dhidi ya Wanawake itakuwa mradi wa miaka kadhaa. Tunatazamia kuanzisha kampeni hii rasmi mwaka huu wa elfu mbili na kumi kwa kuichukua fursa hii kukusanya visa vyako binafsi na wengine mnavyo adhiriwa na Itikadi-za-kijeshi tukitaraji kuwa mchango wako utatuwezesha kubuni mikakati kabambe kutumiwa katika kampeni za usoni. Tafadhali natuungane na CWGL tukafanye bidii kuunga mkono juhudi

Mifano ya maswala yatakayo angaziwa kwenye kampeni:

- *Mjadala wa "Usalama wa Kweli na wa kudumu" na haki za kijinsia.*
- *Jinsi adhari za vita zinavyoadhiri za shughuli za ki-uchumi kwa wanawake.*
- *Wajibu wa kuwahusisha wanawake katika mashauriano ya kutafuta amani, utekelezaji wa mikataba ya amani, diplomasia na katika vyeo vyenye mamlaka ya maamuzi muhimu.*
- *Uingizaji haramu wa silaha ndogo na madhara ya silaha ndogondogo katika vita vya kinyumbani.*
- *Jinsi wanawake wanavyohusishwa katika maafikiano, uponyaji na maridhiano.*
- *Utengenezaji na uuzaji wa silaha katika ngazi za kimataifa.*
- *Vita vya kinyumbani vinavyotekelezwa na wanajeshi.*
- *Dhuluma za kingono na utumwa wa kingono katika maeneo ya mizozo.*
- *Uvunjaji wa haki za kingono na kiuzazi katika maeneo ya mizozo.*
- *Dhuluma za kingono katika majeshi.*
- *Kutochukuliwa hatua za kisheria wanajeshi wanaowadhulumu wananwake.*
- *Unyonge wa wanawake na wasichana wakimbizi nchini za kigeni na wale wa ndani (IDPs).*
- *Wanawake na wasichana wanaoshiriki kwenye mapigano ya kivita.*
- *Ukiukaji wa haki unaotekelezwa na majeshi ya kuweka amani.*
- *Dhuluma kwa wananwake wanaoishi na kufanya kazi mitaani karibu na kambi za kijeshi.*
- *Serikali zinavyotumia nguvu za kijeshi dhidi ya raia na utawanyaji wa makundi yanayotetea demokrasia.*
- *Ubatilizaji wa utawala wa ki-sheria na udunishaji wa haki za kimsingi za kibinadamu kunapotangazwa "hali ya hatari".*
- *Utumiaji wa sheria zakupambana na ugaidi kunyamazisha wanawake watetezi haki za kibinadamu.*
- *Ghasia na mapambano katika jamii.*
- *Uhusiano baina ya Mundo-Jeshi na milengo ya kidini isiyopenda mabadiliko.*
- *Uchafuzi wa mazingira katika operesheni za kijeshi na madhara yake kwa wanawake na watoto.*
- *Uchambuzi wa gharama kukidhi mahitaji ya jeshi baina ya miradi ya kunufaisha jamii.*
- *Kufanyiza kijeshijeshi vikosi vya polisi na umiliki wa vyuo vya kijamii (kama vile shule, mabustani na kadhalika).*
- *Tungetaka kusikia maoni yako!*

iliyoelekezwa, ya kidunia, kuikosoa kwa falsafa ya mfumo wa utetezi wa haki za kike, kukosoa fikra na madhara ambayo Ujeshijeshi huendeleza.

Tunatambua kuwa maudhui ya kampeni hii hayatakuwa maswala rahisi kuangazia, na kuwa baadhi ya wanaharakati huenda wakaibua upinzani katika kazi yao. CWGL inawashauri wanaharakati kutafakari kwa kina usalama wao wanapotekeleza wajibu wa kampeni. Kwa wanaharakati chipukizi katika kampeni, hasa wanaohisi juhudi zao zitafaidi zaidi katika uhamasishaji wa ki-jumla kuhusu dhuluma za kijinsia na haki za kibinadamu; na baadhi ya wale ambao hawawezi kufanya waziwazi kampeni dhidi ya Miundo-Jeshi, CWGL inawahakikishia kuwa itaendelea kuafikisha habari na vifaa muhimu.

VIFAA VYA KAMPENI YA SIKU 16 MWAKA 2010

CWGL inatayarisha vyombo na vifaa vya kampeni vinavyonuiwa kupeana habari kuhusu mada na maoni ya kuratibu kampeni yako. CWGL itawasilisha vifaa vya kampeni ya siku 16 kwenye mtandao kadri tunapokaribia kilele cha kampeni. Unakaribishwa kumuandikia Mshirikishi kupitia anwani hii (16days@cwgl.rutgers.edu) ambaye atakutumia vifaa kwa njia ya posta. Kama ilivyo desturi, vifaa vya ya mada mbalimbali zinazohuhusu dhuluma dhidi ya wanawake vitaendelea kupatikana kwenye tovuti ya Siku 16 kwa manufaa wanaolenga maswala mengine.

Jiunge na vuguvugu la Siku 16 sasa!

Unaweza kuanzilisha au kujiunga na kikundi cha jamii, chuo, juhudi ya kitaifa au kimataifa ya kampeni ya Siku 16. Unaweza pia kuagiza vifaa vya kampeni; unaweza pia kujiandikisha kwenye orodha ya washiriki (jisajili kufuata kiungo hiki kwenye tovuti: https://email.rutgers.edu/mailman/listinfo/16days_discussion; pia unaweza kuitumia ratiba ya shughuli za miaka iliyopita (inapatikana kwenye mtandao) kujipatia mawazo na mbinu mpya kuimarisha kampeni yako; pia unaweza kupata habari zaidi kwa mashirika ambayo yamewahi kuhusika katika kampeni karibu nawe. Huku Novemba ikikaribia, kumbuka kutuma mipango ya shughuli zako za kampeni – na CWGL itaziorodhesha katika ratiba ya shughuli za mwaka 2010 – ili zishirikishwe kama mojawapo ya juhudi za vuguvugu la Siku 16 duniani!

Tembelea tovuti yetu!

Ikiwa ungetaka habari zaidi kuhusu Kampeni ya Siku 16, tafadhali tembelea tovuti yetu kwa kutumia kiungo hiki: https://www.cwgl.rutgers.edu/16days/home.html. Pia unaweza kutazama picha za shughuli za kampeni za awali katika chombo cha Flickr kufuata anwani ya tovuti ifuatayo: http://www.flickr.com/photos/1857851@NO4/.

Tupatane katika Facebook!

Jiunge na kampeni katika Facebook kwa kutafuta "The Official 16 Days of Activism Against Gender Violence Campaign," na ujisajili kuwa shabiki wa kampeni ya Siku 16! Tutakuwa tukikutumia matukio mapya, picha, viungo vya picha za video, na visa vingine vya kusisimua jinsi wanaharakati wanavyoendesha kampeni kote ulimwenguni. Usisahau kuchangia maoni na mawazo yako pia!

Siku 16 za Uanaharakati dhidi ya Dhuluma za Kijinsia ni kampeni ya Kimataifa iliyoanzishwa katika Taasisi ya Uongozi wa Wanawake Ulimwenguni ya kwanza iliyodhaminiwa na Kituo cha Uongozi wa Wanawake Duniani (CWGL) katika Chuo Kikuu cha Rutgers mwaka wa 1991. Walioshiriki walichagua kipindi cha siku kumi na sita kuanzia tarehe 25 Novemba, ambayo ni Siku ya Kimataifa dhidi ya Dhuluma dhidi ya Wanawake, hadi tarehe 10 Desemba, ambayo ni siku ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu, ili kuunganisha dhuluma dhidi ya wanawake na haki za kibinadamu na pia kusisitiza kuwa dhuluma hizo ni ukiukaji wa haki za kibinadamu.

Nakili imetafsiriwa na Bw. Thuku wa Njuguna, Mwanaharakati wa Haki za Kijinsia/Kibinadamu - Men for Gender Equality Now! Kenya

Center for Women's Global Leadership

The 16 Days of Activism Against Gender Violence Campaign is coordinated by the Center for Women's Global Leadership
160 Ryders Lane, Rutgers University, New Brunswick, NJ 08901-8555 USA;
(1-732) 932-8782; cwgl@rci.rutgers.edu; http://www.cwgl.rutgers.edu

RUTGERS
THE STATE UNIVERSITY OF NEW JERSEY